



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**HOTUBA YA MGENI RASMI MH JAMAL KASSIM ALI, WAZIRI
WA NCHI, OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO - ZANZIBAR
WAKATI WA UFUNGUZI WA MKUTANO WA BARAZA LA
WAFANYAKAZI WA MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA
TANZANIA TAREHE 11 FEBRUARI, 2021, ZANZIBAR.**

Dkt. Mussa Juma, Kamishna wa Bima na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi TIRA,
Bi. Khadija I. Said, Naibu Kamishna wa Bima na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi TIRA,
Wawakilishi wa TUGHE Taifa,
Wawakilishi wa TUGHE Mkoa,
Menejimenti ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima,
Ndugu Wajumbe wa Baraza,
Wawakilishi wa Vyombo vya habari,
Ndugu Mabibi na Mabwana

Habari za asubuhi.

Napenda kutumia fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kusafiri salama ili kukusanyika hapa kutekeleza matakwa ya kisheria na utawala bora mahala pa kazi ya kufanya **Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la kujadili Bajeti ya Mamlaka kwa mwaka 2021/22.** Kipekee, napenda kuishukuru Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kwa kunipa fursa ya kujumuika nanyi katika tukio hili la leo, na zaidi kwa kunipa fursa ya kuwa Mgeni Rasmi.

Pia, niwashukuru wanabaraza kwa kuamua kufanya Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi hapa Zanzibar.

Ndugu Wajumbe wa Baraza, Mabibi na Mabwana,

Kipekee niwapongeze sana kwa kufanya mikutano ya Baraza na kuendelea kufuata taratibu za kibajeti na za kiutumishi katika kuleta uwazi na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu ya Mamlaka. Uwepo wa majukwaa kama haya katika taasisi ni chachu ya maendeleo na uelewano katika taasisi.

Natambua kuwa baraza hili ni maalum kwa ajili ya kupitia na kujadili bajeti pendekezwa ya Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Wanabaraza ninawaagiza kupitia bajeti ya Mamlaka katika Mwaka 2021/22 kwa umakini zaidi na kuishauri Menejimenti yenu kuja na mbinu mbadala za kukuza soko la bima. Natambua bado sekta hii ina fursa kubwa ya kutoa mchango katika uchumi wa taifa, niwatake sasa muweke mikakati ya kuanzisha bima ya kiislamu lakini pia ningependa kuona tunatanua wigo wa matumizi ya bima.

Ndugu Wajumbe wa Baraza, Mabibi na Mabwana,

Pamoja na hayo ni vema mkatambua kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati akizindua Bunge la 12 na Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati wa uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi la 10, wote kwa pamoja waliweka mkazo sana katika maendeleo ya shughuli za **Kilimo, Mifugo, Uvuvi na kuvutia Uwekezaji** kuwa sehemu

muhimu katika ukuaji wa uchumi. Kwa dhana hiyo, kuna uhitaji mkubwa sana wa sekta hizo kuingwa na huduma za bima. Hii, itasaidia kuwalinda wananchi dhidi ya majanga yanayoweza kuwakumba.

Ndugu Wajumbe wa Baraza, Mabibi na Mabwana,

Niendeleo kuwa kumbusha tu kuwa sehemu kubwa ya watanzania wanategemea kilimo na Biashara ndogondogo, ni mategemeo ya serikali kuwa kufikia Mwaka 2030, asilimia 10 ya pato ghafi la soko la bima litatokana na kinga katika sekta ya kilimo. Wananchi wengi wanapoteza mitaji na mazao yao katika maeneo hayo. Ni vema wakakingwa kikamilifu na sekta ya Bima.

Ndugu Wajumbe wa Baraza, Mabibi na Mabwana,

Leo mnapojadili utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22 ni muhimu kwenu Wafanyakazi wa Mamlaka ya Bima na Washauri wa Serikali katika masuala ya bima kujikita katika kutafuta majawabu sahihi ya namna bora ya kufikia malengo tajwa katika mipango mbalimbali ya taifa.

Ndugu Wajumbe wa Baraza, Mabibi na Mabwana,

Ninakumbusha na nitaendelea kuwakumbusha, nguvu kubwa ielekezwe kwa wananchi wanyonge. Aidha, Menejimenti ya TIRA, Wafanyakazi pamoja na wadau mnatakiwa kuongeza kasi ya kutoa Elimu kwa Umma. Kwani ni kweli kuwa udumavu wa sekta hii

kunasababishwa na ushiriki mdogo wa watu au umma kwenye shughuli za bima, kwa sababu wengi wetu hatuna elimu ya kutosha ya masuala ya bima. Tuwekeze kwenye elimu zaidi ili kuwafikia wasiofikiwa na kinga mbalimbali za bima, hususan wananchi waishio vijijini.

Ndugu Wajumbe wa Baraza, Mabibi na Mabwana,

Ili yote hayo niliyotaja hapo juu yakamilike kwa haraka na kwa ufanisi, Maslahi ya wafanyakazi kiutendaji na kijamii lazima yaboreshwe ama yawe ni sehemu ya kutoa hamasa kwa wafanyakazi. Vile vile, haki ya mfanyakazi iendane na uwajibikaji kazini. Uwajibikaji wa wafanyakazi ndio unaleta na kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

Ndugu Wajumbe wa Baraza, Mabibi na Mabwana,

Niwahakikishie Menejimenti na Wafanyakazi kwamba, nimechukua yale yote yanayohitaji Wizara yangu kuingilia kati ili kukuza huduma za sekta ya bima, hususan kuidhinishwa kwa Sera ya Bima ya Taifa. Kwa kumalizia, napenda kwa mara nyingine kuwashukuru waandaji na waratibu wa mkutano huu muhimu. Aidha, nawashukuru nyote na nawatakia majadiliano mema na yenye majawabu ya changamoto nilizoziainisha.

Kwa maelezo haya, napenda kutamka kuwa Mkutano wa Sita wa Bazara la Pili la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini umefunguliwa rasmi.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.